

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



**TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI BONDE LA ZIWA
TANGANYIKA**

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi hii kutekeleza majukumu yake ni miaka mitatu.

MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE

Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika itakuwa na mamlaka na majukumu kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi ya Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009. Majukumu hayo ni pamoja na kuandaa mipango ya usimamizi wa Rasilimali za Maji, Miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji; Kuunganisha mipango ya wilaya zilizomo kwenye Bonde katika mipango ya usimamizi wa Rasilimali za Maji; Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi wa miundombinu ya vyanzo vya maji; Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji wa maji na mahitaji ya Rasilimali za Maji; Kuidhinisha kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka; Kumshauri Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kwenye mambo ya kiufundi yahasuyo maji yanayovuka mipaka katika Bonde; Kuteua Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati za vidakio Maji; Kuratibu shughuli za kisekta za ndani za usimamizi wa Rasilimali za Maji katika ngazi ya Bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla.

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya sekta ya maji au sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji,
Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
S.L.P. 456,
40473, DODOMA.

Maombi yaambatishwe wasifu wa mwombaji (CV) na awe na wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika "**Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Tanganyika**" nyuma ya bahasha. Tafadhali tuma nakala ya maombi yako kwa njia ya email kupitia: **ps@maji.go.tz**

Mwisho wa kupokea maombi ni Jumatatu tarehe 6 Januari, 2020 saa 09.30 alisiri

Prof. KitilaMkumbo

KATIBU MKUU

WIZARA YA MAJI

23 Desemba, 2019